# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
| --- | --- |
| | **SEHEMU YA KWANZA** |
| | **MASHARTI YA AWALI** |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Marekebisho ya Sheria mbali mbali. |
| | **SEHEMU YA PILI** |
| | **MAREKEBISHO YA SHERIA YA JUMUIYA NAM. 6 YA 1995** |
| 3. | Kusomwa. |
| 4. | Marekebisho ya kifungu cha 6. |
| 5. | Marekebisho ya kifungu cha 7. |
| 6. | Marekebisho ya kifungu cha 8. |
| 7. | Kuongeza kifungu kipya cha 9A. |
| 8. | Marekebisho ya kifungu cha 11. |
| 9. | Marekebisho ya kifungu cha 13. |
| 10. | Marekebisho ya kifungu cha 15. |
| 11. | Marekebisho ya kifungu cha 19. |
| 12. | Marekebisho ya kifungu cha 24. |
| 13. | Marekebisho ya kifungu cha 26. |
| 14. | Marekebisho ya kifungu cha 27. |

15. Marekebisho ya kifungu cha 29.

16. Marekebisho ya kifungu cha 40.

17. Marekebisho ya kifungu cha 45.

18. Kuongeza kifungu kipya cha 58A.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI NA USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA NAM. 9 YA 2009

19. Kusomwa.

20. Marekebisho ya kifungu cha 4.

21. Marekebisho ya kifungu cha 13.

22. Kuongeza kifungu kipya cha 13A.

23. Marekebisho ya kifungu cha 15.

24. Marekebisho ya kifungu cha 16.

25. Marekebisho ya kifungu cha 19.

26. Marekebisho ya kifungu cha 47.

27. Kuongeza kifungu kipya cha 60A.

28. Kuongeza kifungu kipya cha 57A.

29. Kuongeza kifungu kipya cha 57B.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR, NAM. 8 YA 1999

30. Kusomwa.

31. Marekebisho ya kifungu cha 57.

**SHERIA NAMBA 1 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

7 Mei, 2019

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2019 na itaanza kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika .

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA JUMUIYA NAM. 6 YA 1995

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Jumuiya Nam. 6 ya 1995, katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**4.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Shilingi Laki Mbili" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Milioni Moja".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**5.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika aya (b) kwa kufuta maneno "Shilingi Laki Mbili" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Milioni Moja".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**6.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "Shilingi Laki Mbili" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Milioni Moja".

Kuongeza kifungu kipya cha 9A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 9A mara tu baada ya kifungu cha 9 kama ifuatavyo:

Sifa za Mrajis.

"9A (1) Mtu atakuwa na sifa ya kuchaguliwa kuwa Mrajis akiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ni Mtumishi wa Umma;

(c) mwenye angalau shahada ya kwanza katika fani ya Utawala wa Umma, Sheria, Sayansi ya Jamii au fani nyengine zinahusiana na fani hizo katika Chuo kinachotambulika;

(d) ana uzoefu wa kazi angalau miaka saba katika fani zilizoainishwa katika aya (c) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(2) Msaidizi Mrajis atakuwa na sifa sawa kama za Mrajis"

Marekebisho ya kifungu cha 11.

**8.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya (c) mara tu baada ya aya (b) na kuzipa namba aya nyengine zilizobakia kwa mpangilio uliopo:

"(c) Kumbukumbu za Jumuiya ambazo zitajumuisha majina kamili na saini za wajumbe waanzilishi;"

Marekebisho ya kifungu cha 13.

**9.** Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya (j) mara tu baada ya aya (i) kama ifuatavyo:

"(j) Jumuiya inafanyakazi kinyume na utamaduni wa Zanzibar;"

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**10.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "mitatu" liliopo baina ya neno "ya" na "miezi" na kuweka badala yake neno "miwili"

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**11.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**12.** Kifungu cha 24 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na badala yake kuweka maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**13.** Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**14.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**15.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 40.

**16.** Kifungu cha 40 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

(b) katika kifungu kidogo cha (5) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Marekebisho ya kifungu cha 45.

**17.** Kifungu cha 45 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta maneno "Shilingi Elfu Hamsini" na kuweka badala yake maneno "Shilingi Laki Nne"

Kuongeza kifungu kipya cha 58A.

**18.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 58A mara tu baada ya kifungu cha 58 kama ifuatavyo:

Kufutwa kwa kifungu cha 2(1)(c) cha Sheria nam. 12 ya 2012.

"58A. Kifungu cha 2(1)(c) cha Sheria ya Usajili wa Biashara Nam. 12 ya 2012 kinafutwa.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI NA USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA NAM. 9 YA 2009

Kusomwa.

**19.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 9 ya 2009, katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**20.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa:

(a) Kuongeza mjumbe mmoja mpya katika orodha iliyopo katika aya (k) mara tu baada ya aya (j):

"(k) Waziri anayehusika na masuala ya Wanawake na Watoto."

(b) Kuzipa herufi upya aya (k) hadi (q) kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 13.

**21.** Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "au faini ya Shilingi Milioni Arobaini au adhabu zote mbili faini na kifungo".

Kuongeza kifungu kipya cha 13A.

**22.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A mara tu baada ya kifungu cha 13 kama ifuatavyo :

Katazo la kuchakata na umiliki wa kemikali bashirifu.

"13A. Mtu ambaye kinyume na Sheria anachakata au anamiliki kemikali bashirifu anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini ya Shilingi Milioni Tano au kifungo cha kipindi cha miaka kumi na tano au vyote viwili faini na kifungo."

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**23.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa:

(a) Katika kifungu kidogo cha (1):

(i) katika aya (b) kwa kubadilisha adhabu katika aya ndogo (i) kwa kufuta maneno "kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini na kuweka badala yake maneno "kifungo cha maisha";

(ii) kuweka adhabu moja kwa moja katika aya (c) na itasomeka kama ifuatavyo:

"(c) anavuta, anafukiza, ananusa au vyenginevyo anatumia dawa za kulevya anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili."

(b) Katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta rejea katika aya "(c)" katika orodha na rejea zinazoanzia aya (d) zitabaki kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**24.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) Kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kifuatacho:

"(1) Mtu yeyote ambaye amekiuka sharti lolote la Sheria hii au Kanuni au amri au ruhusa iliyotolewa chini ya Sheria hii, anamiliki kiwango kidogo cha dawa za kulevya bila kujali kitu chochote kilichopo katika sehemu hii atakuwa anatenda kosa:"

(b) Kufuta neno "Tume" katika kifungu kidogo cha (2) linalojitokeza mwishoni mwa kifungu kidogo hiki na kuweka badala yake neno "Waziri".

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**25.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) Kufuta maneno "faini isiyopungua Shilingi Milioni Thelathini na kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi" na kuweka badala yake maneno "kifungo cha maisha na faini isiyopungua Shilingi Bilioni Moja".

(b) Kurekebisha kosa katika rejea "16" kusomeka "15".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**26.** Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (4) kifuatacho:

"(4) Katika uendeshaji wa shauri chini ya Sheria hii, cheti cha uchunguzi kilichoainishwa katika Sheria hii kutoka kwa mchunguzi aliyeidhinishwa na kuweka saini yake kitakuwa ushahidi tosha kwa mambo yaliyoelezwa katika cheti kinachohusiana na dawa za kulevya".

Kuongeza kifungu kipya cha 60A.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 60A mara tu baada ya kifungu cha 60 kama ifuatavyo:

"Kuzuia makosa, usalama kwa kuweka amani na tabia njema.

60A.(1) Hakimu, baada ya kupokea malalamiko au taarifa kwa kiapo dhidi ya mtu yeyote aliyetuhumiwa kuwa anajihusisha katika makosa ya dawa za kulevya, anaweza kumtaka mtu aliyetuhumiwa kujitetea kuwa kwa nini asiamriwe kuweka dhamana kuhakikisha atakuwa na tabia njema kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kama Hakimu atakavyoona inafaa.

(2) Katika kutekeleza uwezo aliyopewa Hakimu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya kifungu cha 60 hadi kifungu cha 74 vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai yatatumika".

Kuongeza kifungu kipya cha 57A.

**28.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 57A mara baada ya kifungu cha 57 kama ifuatavyo:

"Kutumika kwa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu.

57A. Bila kujali sharti lolote katika Sheria hii, Masharti ya Sehemu ya IV, V na VI ya Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu yanaweza kutumika pamoja na mabadilliko ya lazima kuhusiana na utaifishaji chini ya Sheria hii".

Kuongeza kifungu kipya cha 57B.

**29.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 57B mara baada ya kifungu cha 57A kama ifuatavyo:

"Matumizi ya Amri ya kuzuia.

57B. Endapo kutakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba mtu yeyote ametenda kosa lililoainishwa na uchunguzi umeanza kuhusiana na kosa hilo, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuomba Mahakamani amri ya kuzuia kuhusiana na mali yote au mali yoyote ya mtu kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR, NAM. 8 YA 1999

Kusomwa.

**30.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999 katika sehemu hii itajulikana kama Sheria Mama.

Marekebisho ya kifungu cha 57.

**31.** Kifungu cha 57 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya ya (e) mara baada ya aya (d) kama ifuatavyo:

"(e) Sheria ya Chuo cha Kilimo cha Kizimbani Nam. 5 ya 2007".

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Februari, 2019.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***